

---

**Ghorofa ya 7, Jengo la LAMP Pension Fund, Mkabala na Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama  
S.L.P. 72175, Dar es Salaam, Tanzania  
Simu: +255-22 2923513-18; Nukushi: +255-22 2923519**  
Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz) Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

---

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

**TAARIFA KWA UMMA**

**(Imetolewa chini ya kifungu cha 164 cha Sheria ya Mafuta, Sura ya 392)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeanza mchakato wa kutengeneza bei elekezi za gesi asilia kwa ajili ya uwekezaji wa kimkakati nchini Tanzania. Kwa kuzingatia matakwa ya sheria, EWURA imeanzisha taftishi ili kupata maoni ya umma juu ya bei elekezi za gesi asilia kwa ajili ya wawekezaji wa kimkakati nchini Tanzania.

Kama sehemu ya taftishi, mkutano wa wadau kwa ajili ya kupokea maoni juu ya bei elekezi za gesi asilia kwa ajili ya uwekezaji wa kimkakati umepangwa kufanyika katika Ofisi za EWURA siku ya Ijumaa ya tarehe **23 Desemba 2016** katika Ofisi za EWURA zilizopo **Ghorofa ya 7, Jengo la LAMP Pensions Fund, Mkabala na Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama jijini Dar es Salaam** kuanzia **Saa Nne Asubuhi**. Kwa ajili ya majadiliano yenye kuleta tija, andiko juu ya mada ya bei elekezi za gesi asilia inapatikana kupitia tovuti ya EWURA <http://www.ewura.go.tz>. Wadau wote wanaalikwa kuwasilisha maoni yao ifikapo au kabla ya tarehe 27 Disemba 2016.

Maswali au maoni yoyote juu ya mada tajwa hapo juu yawasilishwe kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Mkurugenzi Mkuu**

Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

Ghorofa ya 7, Jengo la LAMP Pension Fund,  
Mkabala na Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama  
S. L. P. 72175, Dar es Salaam  
Simu: +255 (22) 2923513-18  
Nukushi: +255-(022) 2123180

Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz), Tovuti: [www.ewura.go.tz](http://www.ewura.go.tz)